

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPISODE 10: “The Healing Process”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: DAY AT KASSECH

- **Kassech (f, 22)**
- **Askale (f, 21)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE TWO: DAY AT PAPA TILAHUN’S HOUSE

- **Askale (f, 21)**
- **Papa Tilahun (m,76)**
- **Mama Beletu (f,65)**

SCENE THREE: AFTERNOON IN THE HOSPITAL CORRIDOR

- **Papa Tilahun (m,76)**
- **Mama Beletu (f,65)**
- **Aster (f, 15)**
- **Narrator (m, around 35)**

SCENE FOUR: AFTERNOON AT THE HOSPITAL ROOM

- **Aster (f, 15)**
- **Jonas (m, 15)**
- **Papa Tilahun (m,76)**
- **Mama Beletu (f,65)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Askale (f, 21)**
- **Drunkard Minabu (m,55)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo, wapendwa wasikilizaji, na karibu kwenye sehemu ya mwisho ya mchezo wetu “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Katika sehemu iliyopita, Bwana Kasu alimpiga risasi Jonas wakati yeye na marafiki zake walipojaribu kuivamia nyumba ya huyo bwana tajiri. Jonas bado yuko hai lakini amelazwa hospitalini. Marafiki zake wawili pamoja na Bwana Kasu sasa hivi wamo katika kituo cha polisi. Jonas hakujua kwamba huyo bwana aliyempiga risasi ni babake. Wakati huo huo, binti mdogo Aster ameamua kumtafuta Jonas ili amwambie kwamba anampenda. Sehemu ya leo ndio ya mwisho na inaitwa, “MUDA WA KUWEKA MAMBO SAWA.” Tunaanzia nyumbani kwa Kassech. Amepata habari mbaya kumhusu ndugu yake Jonas aliyepigwa risasi na pia ametambua kuwa Bwana Kasu ndiye baba yake mzazi. Ameshtuka si haba kwa mambo yaliyotukia usiku huu.

SCENE ONE: DAY AT KASSECH

1. SFX: DAYTIME AMB, SOUP BOILING

2. **Kassech:** (Sobs) Naam, umesema kweli. Na je kama angeuliwa?

3. **Askale:** Tumshukuru Mungu, hali yake si mbaya. Ana bahati kwa kuwa risasi yenyewe ilibambua sehemu ndogo tu ya paja lake.

4. **Kassech:** Siamini ati Bwana Kasu ndiye baba yetu. Na

baba yangu amempiga risasi ndugu yangu!
SIAMINI!

5. **Askale:** Ni kisa cha kuisimua sana hiki! Hasa nikikumbuka tulipokutana mara ya mwisho, uliniambia huna habari hata kidogo kuhusu nani baba yako.
6. **Kassech:** La kushangaza ni kuwa Papa Tilahun na Mama Beletu waliyajua hayo tangu kitambo!
7. **Askale:** **(Surprises)** Atil? Wote wawili walikuwa wakijua nani baba yako? Kwa nini hawakukuambia?
8. **Kassech:** **(Unhappy)** Si jambo jepesi hivyo, rafiki yangu! Nitakueleza hali yenyewe siku moja penye uzima na uhai. Tutakwenda pamoja hospitalini baadaye?
9. **Askale:** Naam! Nimeshapika chakula cha kumpelekea Jonas. Tutamuomba mtu atutunzie Begidu na Samy; na kisha nitawatunza wote wawili nitakaporudi kutoka hospitalini. Kwa hivyo unaweza kubaki hospitalini kwa muda wote utakaotaka.
10. **Kassech:** Asante, rafiki!
11. **Askale:** Usiwe na wasiwasi! Asubuhi ulimuona Jonas na kama ulivyomuona bila shaka atapona.

Jambo la muhimu zaidi ni yeye kutambua kwamba alitenda kosa kubwa! Anapaswa kurudi nyumbani! Huna budi kumsamehe.

12. Kassech: Jambo hilo kwa kweli limekuwa likinitatiza. Shida ni kwamba Jonas hana mama wa kumpa ushauri (**cries**) na hata ingawa sasa hivi anamjua baba yake, lakini huyo ni baba sampuli gani? Hajawahi kumkimu Jonas hata kidogo: badala yake amempiga risasi! (**Cries more**).

KW BEGIN

13.Askale: Kassech, usilie kwa hisani yako! Ilisadifu kwamba Jonas alitaka kuiba nyumbani kwa babake.

14.Kassech: Askale, mbona maisha yanatuendea vibaya kila mara?

15.Askale: Rafiki yangu, maisha ni magumu kwa kila mtu; jipe moyo.

16.Kassech: Nitajaribu, lakini sasa hivi naona mambo kama yaelekea kutuendea mrama. Hata hivyo, nadhani bora sasa nimakinike na nijipe moyo.

17.Askale: Wazo zuri hilo, Kassech. Ninakuhakikishia kwamba nitakufaa kwa kila hali.

18.SFX: POT IS ABOUT TO BOIL OVER

19. Askale: Tazama chungu chako kisimwage maji jikoni!

20. SFX: COOKING POT'S LID BEING LIFTED

21. Kassech: Asante, rafiki yangu! Uniarifu wakati utakapokuwa tayari kuondoka.

22. Askale: Nitakuarifu! Haya basi tutaonana baadaye!

23. SFX: SOMEONE LEAVES

KW END

24. NARRATION: Watoto hushika mambo wanayoyaona mahali walipo. Kwa hivyo wanahitaji watu walio na mwenendo mzuri. Wakikosa watu wenye mwenendo mzuri wakiwa bado wachanga, ni vigumu sana kuwabadilisha tabia siku za baadaye. Hii ndiyo hali aliyona nayo Jonas. Ukuaji wa mtoto anapokuwa mchanga umegawika katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ni tangu mtoto anapozaliwa hadi anapokuwa na umri wa miaka sita, awamu inayofuata ni kati ya umri wa miaka saba na umri wa miaka kumi na mmoja, na hatimaye, kuna umri wa ubarobaro kuanzia umri wa miaka kumi na miwili na umri wa miaka kumi na minne. Katika kila awamu watoto wana mahitaji yao maalumu. Jonas tayari ameshazivuka awamu zote hizo. Dada yake Kassech amejitahidi kumlea lakini naye pia alikuwa mdogo na alilemewa na majukumu ya kumlea mwanawe wala hakuwa na kipato kikubwa kuikimu familia yake hiyo.

SCENE TWO: DAY, OUTSIDE AT PAPA TILAHUN'S COMPOUND

25. SFX: DAYTIME AMBIENCE

26. **Papa Tilahun:** Mama Beletu! Njoo huku nje!

27. **Mama Beletu:** **(From inside)** Subiri kidogo! Naja, Papa Tilahun.

28. **Papa Tilahun:** **(Angry)** Waja lini?

29. **Mama Beletu:** Nimesema, naja!

KW begin

30. **Askale:** Shikamoo, Papa Tilahun! Naona una haraka.

31. **Papa Tilahun:** **(Gets angry)** Naam, Nina haraka lakini mke wangu amezama huko jikoni! Tunapaswa kuondoka sasa hivi kwenda hospitalini! Alaa! Askale, pole! Hujambo! **(Askale laughs).**

32. **Askale:** Sijambo! Mimi na Kassech pia tunajiandaa kwenda hospitalini.

33. **Papa Tilahun:** Mjukuu wetu ameshatangulia, lakini tunataka kufika huko mapema.

34. **Askale:** Basi tutakutana huko. **(She leaves).**

35. **Papa Tilahun:** Tutaonana baadaye!

36. **Askale:** Baadaye!

KW end

37. **Papa Tilahun:** (To mama Beletu) Mama Beletu! Beletu!
Bele...
38. **Mama Beletu:** (Before he finishes the word, arrives) Naam!
Nishafika.
39. **Papa Tilahun:** Balaa! Mwanamke wewe, yaani hilo jiko lako
huwezi kuliacha hata kidogo.
40. **Mama Beletu:** (Gets angry) Lau si mimi kushughulika humo
jikoni ungekula nini? Ebu nishikie sufuria hii-
nimempikia Jonas chakula.
41. **Papa Tilahun:** Haya, haya. Pole! Nitakubebea.

SCENE THREE: AFTERNOON IN THE HOSPITAL CORRIDOR

42. **SFX: HOSPITAL CORRIDOR**

43. **SFX: ARRANGING A BUNDLE OF ROSES**

44. **NARRATION:** Aster tayari ameshawasili hospitalini Papa Tilahun na Mama Beletu wanapofika. Aster anasimama kwenye ukumbi hospitalini akiwa na fungu la waridi mkononi. Ghafila anawaona babu na bibi yake. Wanaonekana wachovu kwa vitu vyote walivyobeba.

45. **Aster:** Babu, bibi, mnabeba nini?

- 46. Mama Beletu:** Mwenyewe unajua tumemtembelea mgonjwa.
- 47. Papa Tilahun:** Hatujaja likizoni. Mbona hutusaidii?! Umebaki kutukodolea macho! Unashangaa nini?
- 48. Aster:** Subiri hapa, Babu. Kwa hisani yako. Nataka kwenda ndani kwanza nimkabidhi maua haya.
- 49. Mama Beletu.** Sawa! Nenda ukaonane na Jonas. Tutakusubiri hapa lakini usikae kwa muda mrefu!
- 50. Aster:** Sitakaa sana. Babu, wayaonaje maua haya? Yanapendeza?
- 51. Papa Tilahu:** Naam, yanapendeza kama unavyopendeza.
- 52. Aster:** **(Laughs joyfully)** Nisubirini hapa, nitawaita nikishamaliza. **(She is leaving and enters the room).**
- 53. SFX: DOOR OPENS AND CLOSES**

KW BEGIN

- 54. Papa Tilahun:** **(Surprises)** Looo, viijana wa leo wana mambo!
- 55. Mama Beletu:** **(Chuckles)** Nilishajua kitambo.
- 56. Papa Tilahun:** **(Suspicious)** Ulishajua nini kitambo?
- 57. Mama Beletu:** Nilijua sababu ya hiyo simu kupigwa kila mara.

58. **Papa Tilahun:** Ni jambo la wazi! Huwa akiwasiliana na rafiki yake wa dhati, Semira.
59. **Mama Beletu:** Hapana, hapana, hapana!
60. **Papa Tilahun:** Nini basi?
61. **Mama Beletu:** **(In a low voice)** Mjukuu wetu anasumbuliwa na mapenzi.
62. **Papa Tilahun:** Kama ni mapenzi ya dhati, kuna tatizo gani? Mapenzi ya dhati ndio msingi bora wa kujenga familia yenye nguvu. Kama sisi. **(Both laughs)**. Ebu, niambie, nani mwenye bahati?
63. **Mama Beletu:** Mwenye bahati anapokea maua sasa hivi.
64. **Papa Tilahun:** Ati? Una maana kwamba ni huyu Jonas? **(Whispering)** Tuingie ndani.

KW END

65. **NARRATION:** Wakati Aster anapomkabidhi Jonas maua, babu na bibi yake wanajitoma chumbani kisiri. Hata hivyo vijana hao wawili hawatambui kwamba wazee hao wameingia chumbani.

SCENE FOUR: AFTERNOON IN THE HOSPITAL ROOM

66. **Aster:** Sijui nikwambie vipi, Jonas. Ulimi umefunga

kitanzi.

67. **Jonas:** Aster, wewe ni malaika wangu!

68. **SFX: DOOR OPENS SLOWLY IN BACKGROUND**

69. **Aster:** Ninakupenda sana, Jonas!

70. **Jonas:** **(Lovingly)** Na mimi pia ninakupenda, Aster.

71. **Aster:** Unayapenda maua haya?

72. **Jonas:** Naam, ninayapenda!

73. **Papa Tilahun:** Na sisi pia tunayapenda maua hayo **(Laughs from far)**.

74. **Jonas:** Loo! **(Surprised)**

75. **Mama Beletu:** Yanapendeza sana, tena sana!

76. **Aster:** **(A bit embarrassed)** Bibi, babu, ni...

77. **Mama Beletu:** Usione haya, mjukuu wangu.

78. **SFX: DOOR OPEN**

79. **SFX: TWO PEOPLE COME IN**

80. **SFX: DOOR CLOSE**

81. **Papa Tilahun:** Alaa! Kassech.
82. **Mama Beletu:** Askale, nyote mmewasili wakati mwafaka.
83. **Kassech:** Hujambo! Kuna nini ?
84. **Askale:** Hujambo! Aster, unaonekana mchovu!
85. **Aster:** **(Embarrassing)** Sijambo.
86. **Mama Beletu:** **Jana usiku hakulala.**
87. **Papa Tilahun:** Hapana, anaona haya kidogo.
88. **Aster:** **(Still embarrassed)** Babu!
89. **SFX: DOOR OPEN**
90. **SFX: SOMEONE ENTERS**
91. **SFX: DOOR CLOSE**
92. **Minabu:** Nani anaona haya kidogo? Natumai si mimi.
(He laughs, everyone laugh).
93. **Papa Tilahun:** Alaa! Bwana Minabu. Karibu! Sidhani unalo la kuonea haya sasa. Umeshaacha kunywa pombe. **(Still laughing).**
94. **Minabu:** Tazama hili kovu kwenye paji langu la uso. Mimi na ulevi sasa hivi kama mbingu na ardhi tulivyotengana! **(All laughs).**

- 95. Papa Tilahun:** Kassech, jana usiku tulizungumza na baba yako Bwana Kasu katika kituo cha polisi. Anajuta sana alivyotenda.
- 96. Mama Beletu:** Watamwachilia hivi karibuni. Wakili wake ameshikilia kwamba alitenda aliyoyatenda kwa kujihami.
- 97. Minabu:** Sasa ndo wakati wa kubadilisha mienendo yetu. Tunahitajika kubadilisha mambo yetu kwa ajili ya watoto wetu!
- 98. Papa Tilahun:** Ninapenda huo msemu wako, "Sasa ndo wakati wa kubadilisha mienendo yetu." Nadhani ndiyo sababu wewe ukawa wa kwanza kubadilisha mienendo. **(All laughs).**
- 99. Minabu:** Natumai sijachelewa – lau ningekuwa nilibadilika kitambo singekuwa na kovu hili kwenye kovu.
- 100. Papa Tilahun:** Penye uzima na uhai, hutapata makovu mengine kwenye paji lako la uso.
- 101. Minabu:** Naam, Papa Tilahun. Sitayapata TENA! **(All laugh).**
- 102. Kassech:** Jamani! Tusimsahau mgonjwa wetu.

103. Askale: Usiwe na wasiwasi, anatunzwa vizuri. Au siyo, Aster? **(All laugh).**

OUTRO:

Tumefika mwisho wa hadithi yetu “MWANA MPOTEVU- KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”, ulioandikwa na Mantegaftot Sileshi Siyoum. Kwenye sehemu ya leo hakuna mhusika anayelia! Tumewashuhudia vijana wawili wapenzi na Minabu aliyekuwa mlevi wa kutupwa, wakitoa ahadi. Vipi wewe? Unafikiriaje kuhusu malezi ya mapema ya mtoto? Je unakubaliana nasi kuwa ni muhimu kuwalea watoto kwa njia nzuri na kuwahimiza waulize maswali ili wajifunze? Ukitaka kusikiliza tena sehemu hii na sehemu nyingine za mchezo wetu, fungua ukurasa wa tovuti wa dw.de/lbe. Kwaheri kwa sasa!